

**KUMB NA: ISS/JI/2020**

JINA LA MWANAFUNZI.....

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ILUNGU MWAKA 2020**

**1.0 UTANGULIZI**

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii kwa mwaka 2020/2021. Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe 06/01/2020 unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 06/01/2020.

**2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**A. SARE ZA SHULE**

**I. WASICHANA**

- Blauzi 2 nyeupe mikono mifupi
- Sketi 2, damu ya mzee na kaki ziwe na marinda mengi yasiyopungua 16 na yasiyozidi 20
- Viatu vyeusi vya kamba vya ngozi visivyoye na kisigino kirefu (siyo bajaji)
- Sweta damu yam zee
- Soksi nyeupe

**II. WAVULANA**

- Shati 2 nyeupe mikono mifupi
- Suruali 2, damu yam zee na kaki ziwe na marinda(zisiwe modal/flat front)
- Viatu vyeusi vya kamba vya ngozi visiwe na visigino virefu (siyo bajaji)
- Soksi nyeusi

**2.1 SARE ZA MICHEZO**

- Tracksuit bluu yenye mistari nyeupe pembeni
- Viatu vya michezo (raba za kamba)

**2.2 VIFAA VYA KUJIFUNZIA**

- Daftari kubwa 9 counter books quire 3, mkebe, rula na kalamu (wino na risasi)

**3.0 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE**

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu namba 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu nchini. Unapaswa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:

- a. Heshima kwa viongozi , wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wenzako na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- b. Mahudhurio mazuri katika shughuli za ndani na nje ya shule ni muhimu
- c. Kuhudhuria masomo ya zida (remedial studies)
- d. Kuwahi katika shughuli za shule na shughuli nyingine utakazopewa
- e. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- f. Kutunza usafi wa mwili, mvazi na mazingira ya shule
- g. Kuvaa sare za shule wakati wote unapotakiwa
- h. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

### **3.1 MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI AKAFUKUZWA SHULE /KUSIMAMISHWA MASOMO**

1. Wizi
2. Uasherati, ubakaji na ushoga
3. Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya, kama vile bangi na pombe
4. Kupigana
5. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
6. Kudharau bendera na wimbo wa taifa
7. Kuo au kuolewa
8. Kupata au kusababisha mimba ndani au nje ya shule
9. Kutoa mimba
10. Kugoma, kuchochea au kuongoza mgomo au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
11. Kugomea adhabu
12. Utoro wa muda mrefu
13. Kukutwa na simu
14. Kulala rumande (polisi/mahabusu) kwa kosa la jinai
15. Kukutwa kwenye maeneo ya starehe kama vile kumbi za disco, baa, pool table nk.
16. Kuhifadhi wahalifu
17. Kukaa magengeni wakati wote na kushirikiana na makundi ya kihalifu
18. Kupaka rangi, mfano kucha, uso nk
19. Kwenda kwenye nyumba za walimu bila kibali maalumu
20. Kuvaa mavazi yasiyo ya heshima ndani na nje ya shule
21. Kudharau walimu, wazazi/walezi

### **3.2 MAMBO YA KUZINGATIA**

- a. Fomu ya upimaji afya (medical examination form) ambayo itajazwa na mganga. Fomu hii itarejeshwa mwanafunzi anaporipoti shuleni
- b. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na uongozi wa shule.

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI ILUNGU!**

.....  
 KIPOROZA, C.  
 Mkuu wa shule

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI  
HALMASHAURI YA WILAYA YA MBEYA  
SHULE YA SEKONDARI ILUNGU  
FOMU YA AHADI YA MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI**

**A. SEHEMU YA MWANAFUNZI**

Mimi ..... msichana /mvulana. Ninakubali kujiunga kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Ilungu. Nitatii sheria zote za shule na nitaishi maisha mazuri nay a mfano. Nitakuwa mwanafunzi mwenye nidhamu, bidii katika masomo na kazi nyingine.

**B. SEHEMU YA MZAZI/MLEZI**

Mimi..... ninakubali mtoto wangu..... asome katika shule ya sekondari Ilungu. Ninaahidi kumtimizia mahitaji yote muhimu kama ilivyoagizwa. Nitatoa ushirikiano wa dhati katika maendeleo ya motto wangu kitaaluma na kinidhamu.

Sahihi ya mzazi/mlezi..... tarehe..... namba ya simu.....

**C. KWA MATUMIZI YA OFISI TU**

Mwanafunzi.....amepokelewa shuleni tarehe.....sahihi.....

MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE AND TECHNOLOGY  
MBEYA DISTRICT COUNCIL

Ilungu secondary school  
P.O.Box 2957  
**MBEYA**  
06/01/2020

Ref. No. ISS/JI/2019

Medical In-charge

..... (Name of hospital)

P.O. Box .....

**MBEYA**

**RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

Please examine ..... (Name of student) as to his/her fitness for pursuing studies at this school

1. Hemoglobin.....
2. P.V bleeding.....
3. Blood pressure.....
4. Blood group.....
5. (a) Sight.....  
(b) Hearing .....
6. Urine for sugar & pregnancy test .....
7. Stool for routine .....
8. Skin disease.....
9. Asthma.....
10. Epilepsy .....
11. Pulmonary Tuberculosis.....
12. Leprosy.....
13. Deformity .....
14. V. D (Give type) .....
15. Mental problems .....
16. Any other serious disease not mentioned above

.....  
.....

**COMMENTS**

.....

NAME OF DOCTOR.....SIGNATURE.....

STAMP.....